TANGAZO LA SERIKALI NA. 623 la tarehe 1/9/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 28(3))*

AMRI YA NAULI ZA ABIRIA NA MIZIGO KATIKA NJIA YA KIWIRA-MBAMBA BAY KATIKA ZIWA NYASA YA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Nauli za Abiria na Mizigo Katika Njia ya Kiwira-Mbamba Bay Katika Ziwa Nyasa ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Amri hii itatumiwa na meli zinazomilikiwa na Kampuni wakati zikitoa huduma ya usafirishaji abiria na mizigo maeneo ya Tanzania katika Ziwa Nyasa.

Tafsiri

3. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 415

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

Sura ya 212

"Kampuni" maana yake ni Kampuni ya Huduma za Meli iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni;

"Shirika" maana yake Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

"meli" maana yake ni meli zinazoendeshwa na Kampuni katika Ziwa Nyasa.

## SEHEMU YA PILI
## NAULI NA MASHARTI YANAYOTUMIKA

Nauli zilizoidhinishwa

4. Kampuni inayoendesha meli-

(a) itatoza nauli ya abiria na mizigo isiyozidi viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na Jedwali la Pili katika Amri hii;

(b) itatunza taarifa za ubebaji wa abiria na mizigo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo udhibiti;

(c) itazingatia masharti ya utoaji huduma ya usafiri kwa njia ya maji yaliyotolewa na Shirika kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Majini. (Sura ya 165)

Masharti ya huduma

5. Wakati wa kutoa huduma, Kampuni itazingatia masharti yafuatayo:

(a) itatoa tiketi kwa abiria zinazoonesha nauli isiyozidi viwango vilivyoidhinishwa;

(b) itatoa tiketi kwa abiria wakiwa nje ya meli ili kukidhi matakwa ya usalama majini;

(c) itapima uzito wa mizigo ikiwa nje ya meli ili kukidhi matakwa ya usalama majini;

(d) itazingatia ratiba ya safari za meli kama ilivyotolewa na kampuni kwa wateja; na

(e) itazingatia viwango vya usalama kama vilivyoainishwa katika Sheria ya Usafiri Majini na kanuni zake. (Sura ya 165)

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya 4(a))*

**NAULI KIKOMO ZA ABIRIA ZILIZOIDHINISHWA KWA AJILI YA NJIA YA KIWIRA-MBAMBA BAY**

| Njia | VIP I (TZS) | VIP II (TZS) | DARAJA LA PILI (TZS) | DARAJA LA TATU (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| Kiwira – Ifungu | 18,600 | 16,600 | 10,800 | 4,500 |
| Kiwira – Manda | 27,900 | 20,600 | 15,600 | 9,600 |
| Kiwira – Mkili | 33,200 | 26,600 | 18,600 | 10,900 |
| Kiwira - Mbamba Bay | 45,600 | 35,800 | 25,600 | 17,300 |
| Nsisi – Manda | 18,600 | 16,600 | 10,800 | 5,800 |
| Nsisi – Mkili | 27,900 | 24,800 | 18,600 | 8,300 |
| Nsisi - Mbamba Bay | 35,800 | 30,600 | 21,900 | 10,900 |
| Manda – Mkili | 18,600 | 16,600 | 10,800 | 5,800 |
| Manda - Mbamba Bay | 27,900 | 20,600 | 18,600 | 9,600 |
| Njambe - Mbamba Bay | 18,600 | 16,600 | 10,800 | 4,500 |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya 4(a))*

**NAULI KIKOMO ZA MIZIGO ZILIZOIDHINISHWA KWA AJILI YA NJIA YA KIWIRA-MBAMBA BAY**

| Bidhaa | Kipimo | Kiwango (Tsh) |
|---|---|---|
| Kichele/ Bidhaa zinazochukua nafasi kubwa | tani | 50,000 |
| Godoro | moja | 1,500 |
| Pikipiki/Baiskeli | moja | 10,000 |
| Gari | tani | 35,000 |

| **Bidhaa** | **Kipimo** | **Kiwango (Tsh)** |
|---|---|---|
| Wanyama/Ndege | kasha la wanyama | 20,000 |
| Bidhaa nyingine | tani | 20,000 |

Dar es Salaam
1st August, 2023

KAIMU ABDI MKEYENGE
*Mkurugenzi Mku*